# KCPE REVEALED

## MTIHANI WA KITAIFA

## UBASHIRI SHESHE

Pinpoint Publishers
Enriching your knowledge

206504

Saa 1 Dak. 40

## - KISWAHILI - LUGHA - 2021

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika hii ya maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**

**JINA LAKO**

**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku nyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengewa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari kwenye kisanduku chenye herufi uliochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

23. Tegua kitendawili kifuatacho.
Ukimcheka anakucheka, ukimwomba anakuomba ______
A. kioo B. mwangwi C. kivuli D. kasuku.
**Katika karatasi ya majibu**, jibu sahihi ni B mwangwi.
**23** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 23, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri, kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

FUNGUA UKURASA

Pinpoint
*Email: pinpointpublishers10@gmail.com*

Covid-19 Epuka kutangamana kwa karibu na watu

KCPE REVEALED NATIONAL EXAMINATIONS

***Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Wakazi wa eneo la Funzi ___1___ asubuhi na mapema. Walikuwa wamejiandaa ili ___2___ katika uchaguzi wa viongozi wengine. Asilimia kubwa ya wakazi hao ___3___ kwa kutumia magari ya umma. Akina Juma walipoingia ndani ya basi, ___4___ aliupiga ubavu wa gari kisha wakaondoka. Waliwasili uwanjani pale wakati wa ___5___, jua la utosini lilikuwa limewaka mno. ___6___ ya wagombeaji walipatikana katika sakata ya kuwapiga wapigakura ___7___. Wengine walikamatwa na kuondolewa pale wakisubiri kufunguliwa mashtaka. Akina Juma walipokuwa wakirudi nyumbani, gari lao lilihusika katika ajali. Kwa bahati nzuri hakuna aliyeaga dunia ila majeraha madogomadogo tu. Haukupita muda mrefu kabla ya gari lao kuanza ___8___ moshi. Hatimaye moto mkubwa ulizuka, gari lote liliteketea likawa majivu. Hakika, ___9___.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | walidemka | walijihimu | walifumukana | walifumuka |
| 2. | kushurutishwa | kujiingiza | kushiriki | kujihimiza |
| 3. | ilisafirisha | walisafirisha | walisafiri | ilisafiri |
| 4. | kondakta | utingo | manamba | taniboi |
| 5. | macheo | alasiri | adhuhuri | machweo |
| 6. | Dhidi | Kati | Baadhi | Minghairi |
| 7. | kumbo | konde la nyuma | butwaa | fagio la chuma |
| 8. | kuvuka | kufuka | kufuma | kuvuma |

9. **A.** hakuna bamvua lisilokuwa na usubi **B.** hakuna marefu yasiyokuwa na ncha
**C.** hakuna masika yasiyokuwa na mbu **D.** hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe

Ama kwa ___10___, juhudi za serikali kutetea haki za watoto zimeanza kuzaa matunda. Kila mtu katika jamii ameanza kumthamini kila mtoto. Hakuna tena anayetaka ___11___ mtoto yeyote, awe msichana au mvulana. Hatua ___12___ imebadilisha jinsi watoto ___13___ na kujichukulia. ___14___ waliokuwa wakijidharau sana wanajiheshimu na kujiona bora. Hata hivyo, huo sio mwisho wa mambo. Serikali ingali ___15___ jamii kuendelea kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata haki zao.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 10. | hakika | vile | sababu | kuwa |
| 11. | kumstahi | kumtweza | kumkweza | kumtwaza |
| 12. | zile | hizo | hii | hiyo |
| 13. | wanavyojiona | wanaojiona | watakavyojiona | wanavyoonana |
| 14. | Wenye | Kwingi | Wingi | Wengi |
| 15. | itaihimiza | imeihimiza | inaihimiza | ingaliihimiza |

**16.** Tambua kielezi katika sentensi ifuatayo.
**Sokoni pale pamejengwa duka chini ya mti.**
A. sokoni B. chini ya mti
C. pale D. chini ya

**17.** Chagua orodha yenye nomino zinazopatikana katika ngeli moja.
A. mchungwa, mvua, mkono
B. miwani, mikunga, mifugo
C. mafua, mapishi, makufuli
D. chungu, chura, chawa

**18.** Chagua jibu lenye kitenzi kilichoundwa kutokana na nomino.
A. cheza-mchezo B. urembo-rembesha
C. mtoto-utoto D. boreka-boresha

**19.** Kiunganifu –a kimetumikaje katika sentensi ifuatayo? **Mlinzi wa hasira amefutwa kazi.**
A. Kuonyesha umilikaji
B. Kuonyesha tabia
C. Kuonyesha aina
D. Kuonyesha cheo

**20.** Chagua maelezo ambayo ni kweli kuhusu neno **`changarawe'**.
A. Lina herufi nane.
B. Lina sauti tisa.
C. Lina herufi kumi.
D. Lina silabi nane.

**21.** Jibu lipi lililounganisha sentensi zifuatazo kwa usahihi?
**Yohana alipewa zawadi. Yohana hakufurahi.**
A. Yohana angepewa zawadi angefurahi.
B. Yohana alipewa zawadi licha ya kufurahi.
C. Ingawa Yohana alipewa zawadi hakufurahi.
D. Yohana alipewa zawadi maadamu hakufurahi.

**22.** Chagua sentensi iliyotumia kitenzi katika kauli ya kutendesha.
A. Matunda yaliyooza yametupwa.
B. Pangusa meza hiyo vizuri.
C. Mama ameyatokosa mahindi yale yakaiva.
D. Ng'ombe wale wamekimbizwa na simba.

**23.** Chagua wingi wa;
**Mgonjwa wa kifuakikuu amepelekwa kwa tabibu.**
A. Wagonjwa wa kifuakikuu wamepelekwa kwa tabibu.
B. Wagonjwa wa vifuavikuu wamepelekwa kwa matabibu.
C. Wagonjwa wa kifuakikuu wamepelekwa kwa matabibu.
D. Wagonjwa wa vifuavikuu wamepelekwa kwa matabibu.

**24.** Nuru alipokuwa akielekea shuleni wakati wa subuhi, jua lilikuwa nyuma yake. Je, shule ilikuwa upande gani wa dira?
A. magharibi B. mashariki
C. kusini D. kaskazini

**25.** Orodha gani yenye vitenzi pekee?
A. andika, ukumbusho, kimbia
B. uguza, ona, imba
C. vizuri, mbaya, mrefu
D. changu, wako, zake

**26.** **Kitu unachoona kuwa hakina manufaa yoyote kwako kinaweza kumfaa mwingine kabisa.** Chagua methali inayoafikiana na maelezo haya.
A. Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno.
B. Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.
C. Bura yangu siibadili na rehani.
D. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.

**27.** Yakobo alikuwa na mazoea ya **kuwategemea** sana wenzake, hatimaye **aliteseka** sana maishani. Chagua nahau zinazoweza kutumika badala ya maneno yaliyokolezwa rangi.
A. kuwa kupe, alikula mwande
B. kuenda nguu, alikula mwata
C. kujipalia makaa, alilia ngoa
D. kutia mrija, alikula mumbi

**28.** **`panda, kaa, chupa** na **paa'** ni mifano ya;
A. visawe B. vitate
C. vitawe D. vitanzandimi

**29.** Maamkuzi gani ambayo hutumika wakati wa jioni pekee?
A. sabalheri
B. masalheri
C. chewa
D. hujambo

**30.** Chagua ukanusho wa, Nyumba ambayo ilijengwa imepakwa rangi.
A. Nyumba ambayo haikujengwa haijapakwa rangi.
B. Nyumba ambayo ilijengwa haikupakwa rangi.
C. Nyumba ambayo ilijengwa haijapakwa rangi.
D. Nyumba isiyojengwa haijapakwa rangi

***Soma kifungu hiki kisha uyajibu maswali 31-40.***

Ugonjwa ni kitu kinachosababisha mmea, mtu au mnyama kuwa katika afya mbaya. Magonjwa ni kati ya matatizo sugu ambayo serikali yetu inajaribu juu chini kushindana nayo. **Ni nani anayependa kuwa mgonjwa?** Hakuna anayependa, kwa kuwa ugonjwa ni kikwazo na ni chanzo cha gharama. Unapokuwa mgonjwa, huhisi tu vibaya bali pia huenda ukashindwa kwenda kazini au shuleni, kutafuta pesa au kuitunza familia yako. Huenda hata ukahitaji mtu fulani akutunze na kulipia gharama za dawa na matibabu. Kuna msemo usemao **"Kinga ni bora kuliko tiba."** Baadhi ya magonjwa hayaepukiki. Hata hivyo, bado kuna mambo mengi unayoweza kufanya ili kupunguza au hata kuzuia kuanza kwa ugonjwa. Mambo gani unayoweza kufanya ili kuwa na afya bora?

Si suala la mjadala tena kuwa njia moja bora zaidi ya kujikinga na ugonjwa na kuepuka kueneza ugonjwa ni kunawa mikono. Ni rahisi kupata homa au mafua kama utagusa pua au macho yako huku mikono yako ikiwa na viini. Njia bora ya kujilinda na maambukizi ni kunawa mikono yako kwa ukawaida. Kudumisha usafi kunaweza pia kuepusha kuenea kwa magonjwa hatari kama vile nimonia na kuendesha, ambayo kila mwaka husababisha vifo vya watoto zaidi ya milioni mbili, walio chini ya umri wa miaka mitano. Hata kuenea kwa ugonjwa hatari wa Korona, kunaweza kupunguzwa kwa kuwa na ukawaida wa kunawa mikono.

Usifikiri kwamba kunawa mikono yako kikamilifu ni jambo lisilo muhimu. Uchunguzi umeonyesha kwamba asilimia kubwa ya wale wanaotumia vyoo vya umma hawanawi mikono yao vizuri au hawanawi kabisa. Unapaswa kunawa mikono yako jinsi gani? Lowesha mikono yako katika maji safi ya bomba na kisha utumie sabuni. Sugua mikono yako pamoja ili kupata povu, bila kusahau kusafisha kucha, vidole, pande zote za mkono na katikati ya vidole vyako. Endelea kusugua kwa sekunde ishirini hivi. Safisha mikono yako katika maji safi yanayotiririka. Kausha mikono yako kwa kutumia kitambaa safi au karatasi ya kukaushia mikono.

Ni rahisi kufanya mambo hayo, na kufanya hivyo kunaweza kuzuia ugonjwa na kuokoa uhai. Katika maeneo fulani **ni muhali** kupata maji safi ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Hata hivyo, kutopatikana kwa maji safi kunaweza kuwa tatizo popote ulimwenguni. Hili huweza kutokea ikiwa chanzo kikuu cha maji safi ya kunywa kitachafuliwa kutokana na mafuriko, kimbunga, kuharibika kwa bomba au jambo lingine lolote. Ikiwa chanzo cha maji si safi au hakijatunzwa vizuri, maji yanaweza kusababisha magonjwa yanayotokana na vimelea, kama vile kipindupindu, ugonjwa hatari wa kuendesha, homa ya matumbo, mchochota wa ini na magonjwa mengine. Maji yasiyo salama ni moja ya chanzo cha ugonjwa wa kuendesha kwa visa vya watu zaidi ya bilioni moja kila mwaka.

Mara nyingi mtu huambukizwa ugonjwa wa kipindupindu baada ya kunywa maji machafu au kula chakula kilicho na viini kutoka kwa watu walioambukizwa. Unaweza kuchukua hatua gani ili kujilinda hata baada ya kupatwa na ugonjwa au maambukizi mengine yanayotokana na maji yasiyo salama? Hakikisha kwamba maji unayokunywa, unayotumia kusafisha meno, kugandisha barafu, kusafisha chakula na vyombo au kupikia, yanatoka kwenye chanzo salama. Chanzo salama ni kama vile bomba la umma, lenye maji yaliyowekwa dawa ili kuua viini au maji ya chupa yanayotengenezwa na kampuni inayoaminika. Ikiwa maji ya bomba unayotumia si safi, chemsha maji kabla ya kutumia au weka dawa ya kuua viini. Unapotumia kemikali au dawa za kuua viini katika maji kama vile klorini au dawa za kusafisha maji, fuata maelekezo ya watengenezaji.

Tumia mashine ya kuchujia maji iliyo bora ikiwa inapatikana na ikiwa unaweza kununua. Ikiwa hakuna dawa za kuua viini katika maji, tumia dawa ya kuondoa madoa, weka matone mawili katika lita moja ya maji, changanya vizuri kisha uache maji yatulie kwa dakika thelathini kabla ya kuyatumia. Siku zote hifadhi maji safi katika vyombo vilivyo safi na ufunike ili kuzuia yasichafuliwe kwa njia yoyote. Aidha, hakikisha kwamba vyombo vinavyotumiwa kuchota maji kama vile kikombe ni safi. Mikono yako inapaswa kuwa safi unapotumia au unapogusa vyombo vinavyotumiwa kutunza maji na usitumbukize mikono yako au vidole katika maji ya kunywa.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, hakuna anayetaka kuwa mgonjwa kwa kuwa;
A. mgonjwa ni kikwazo na chanzo cha gharama.
B. maradhi huzuia utendaji wa mambo mengi.
C. maradhi ni chanzo na kikwazo cha gharama.
D. magonjwa hufanya mtu akose mtu wa kumtunzia familia yake.

**32.** Magonjwa huweza kuathiri yafuatayo **isipokuwa;**
A. elimu B. uchumi
C. familia D. makazi

**33.** Kauli **"Kinga ni bora kuliko tiba"** ina maana kuwa;
A. ubora wa kinga yoyote hutegemea uwezo wake wa kutibu.
B. ni vyema kuyakinga magonjwa yatokeapo kabla ya kuyatibu.
C. ni vyema kuzuia kutokea kwa jambo badala ya kutatua athari zake.
D. ni vigumu kutibu magonjwa ambayo hayakingiki.

**34.** Mwandishi wa makala haya anapouliza, **'Ni nani anayependa kuwa mgonjwa?'** anamaanisha kuwa;
A. ana uhakika kwamba hakuna yeyote anayetamani kuwa mgonjwa.
B. angependa kujua iwapo kuna mtu ambaye angependa kuwa mgonjwa ili amshauri.
C. anaelewa kuwa wanaotamani kuwa wagonjwa ni watu wachache.
D. anatambua kuwa mtu asiyejua madhara ya ugonjwa anaweza akapenda kuwa mgonjwa.

**35.** Kifungu kinadokeza kuwa magonjwa hatari kama vile nimonia na kuendesha;
A. husababisha vifo vya watoto milioni mbili kila mwaka.
B. husababishwa na kutodumisha usafi.
C. husababisha vifo vya watoto zaidi ya milioni mbili, walio chini ya umri wa miaka mitano humu nchini.
D. hudumishwa kwa kuendeleza usafi.

**36.** Kulingana na aya ya tatu, vitu gani ambavyo ni lazima viwepo ili kusafisha mikono?
A. maji, sabuni, bomba
B. sabuni, kitambaa, maji
C. kitambaa, karatasi, sabuni
D. bomba, kitambaa, sabuni

**37.** Maneno **'ni muhali'** yana maana gani jinsi yalivyotumika katika kifungu?
A. Ni kawaida
B. Ni ajabu
C. Ni vigumu
D. Ni rahisi

**38.** Kulingana na kifungu, ugonjwa wa kipindupindu huweza kuzuiwa kupitia;
A. kuzingatia hali ya juu ya usafi.
B. kula chakula ambacho hakina uchafu.
C. kunywa maji yaliyo safi.
D. kuepuka viini kutoka kwa watu walioambukizwa.

**39.** Makala haya yanashauri kuwa;
A. matumizi ya kemikali za kusafisha maji yazingatie maelekezo ya watengenezaji.
B. matone mawili ya dawa ya kuondoa madoa ndiyo bora zaidi ya kuua viini.
C. mara nyingi maji yanafaa kuhifadhiwa katika vyombo vilivyo safi na kufunikwa ili kuzuia yasichafuliwe kwa njia yoyote.
D. mikono inafaa kusuguliwa kwa dakika ishirini hivi ili kuwa safi.

**40.** Chagua kichwa bora zaidi kwa makala haya.
A. Magonjwa Mbalimbali.
B. Faida za Usafi.
C. Mchango wa Usafi katika Kuzuia Magonjwa.
D Madhara ya Magonjwa.

***Soma kifungu hiki kisha uyajibu maswali 31-40.***

Bwana Limbuka alikuwa amekuzwa katika mazingira ya kazi nyingi. Wazazi wake waliamini kuwa mtu akifunzwa kazi mapema, atakuwa mkakamavu maishani. Kwake Limbuka alichukulia kinyume. Kimoyomoyo alijiambia kuwa akipata kazi na aoe, kisha apate watoto, hatawasumbua. Alitia bidii shuleni na akapita mitihani yake ya viwango vya juu. **Baadaye akabahatika kama mtende**, akavuka mabonde na milima hadi huko ughaibuni kuongezea masomo.

Akiwa bado ana dukuduku lake la hapo awali, aliziangalia familia za huko na kuvutiwa. Akathibitisha kuwa makuzi ya kikwao ni ya kishamba. Akasahau kuwa kisomo cha kijadi alichopewa kilikuwa ndicho chanzo cha ufanisi wake.

Baada ya miaka si haba, alirudi kwao, akaoa na kujaliwa watoto wawili. Alimwapia mkewe kuwa yeye hatathubutu kushikilia makuzi ya kizamani. Hakuelewa kuwa **jambo usilolijua ni usiku wa giza.** Hapo basi wakawalea watoto kama mayai. Watoto walipoguswa kidogo, walishtakia hali kwa wavyele wao, nao waliwabwekea 'wachokozi' kwa hasira. Watu wakabakia macho tu! Wakamngojea "msema kweli wa maisha". Watoto wakaota pembe za kinyati. Kwa kukosa kazi yoyote, waliigiza lolote lile waliloliona katika runinga. Waliropokwa ovyo popote pale bila tahayuri yoyote. Walipokua kidogo walianza kunywa pombe, kuvuta sigara na kutumia dawa zingine za kulevya.

Vituko vilipozidi na kuvuka mipaka, walianza kuwadharau na kuwaaibisha wageni maskini waliowatembelea huko kwao. Waliowahi kufika kwao kwa vigari vya supana mkononi walichekwa. Hata watoto walishangaa walipoona watu wakipanda 'matatu" au "mabasi". Walipokwenda kuchukuliwa shuleni kwa gari walilolipuuza, walijificha na kusema, "Hilo ni gari la sokoni, halitufai." Walipoingia kwenye maduka, walichagua bidhaa ghali. Bwana Limbuka na mkewe walikidhi matakwa ya wana wao wakidhani kuwa huko ndiko kupenda. Walisahau kuwa kuna leo na kesho. Walisikika wakisema, "watoto safi sana hawa. Ni jasiri na werevu. Hawana undani wowote." Hawakukumbuka kuwa kuna yale yanayofaa kusemwa na kuna yale ya kumezea. Maneno mengine huchoma watu nyoyoni.

Watoto wa Limbuka walizidi kudidimia kisimani. Shule nayo ikawapiga chenga. Walishindwa mitihani yao ya kidato cha nne. Katika hali ya kuokoa jahazi lililokuwa likizama, wazazi waliwapa mitaji ya kuanzishia biashara. Baada ya muda mfupi mambo yalivurugika. Mali yote yalifujwa kwa kasi kwani buyu la asali halichovwi mara moja. Hatimaye ukata uliwanyemelea, wakawa maskini hohehahe wasioweza hata kuwasaidia wazazi wao wazee. Walibaki kuwayawaya na kuwazubaisha walimwengu. Limbuka na mkewe nao walijifunza kuwa mtoto hakuzwi kwa kubwagiwa mapesa na kuengwaengwa. Anafaa kufunzwa jinsi ya kuukabili ulimwengu bila kutegemea nundu za wazazi. Mtegemea cha ndugu hufa maskini.

**41.** Kulingana na **aya ya kwanza**, ni kweli kuwa;
A. Bwana Limbuka aliwakuza watoto wake katika mazingira ya kazi nyingi.
B. Limbuka alikua kinyume na alivyokuzwa.
C. Limbuka alifanya kazi alizopewa na wazazi wake bila kupenda.
D. Limbuka alifanya kazi alizopewa na wazazi wake bila kupenda.

**42.** Kulingana na aya ya pili, mhusika alisahau kuwa;
A. asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
B. mwacha mila ni mtumwa.
C. majuto ni mjukuu huja baadaye.
D. mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

**43.** Kulingana na aya ya nne, maneno yaliyosemwa na watoto wanaozungumziwa yalikuwa;
A. ya uongo
B. ya ukweli
C. ya kuchoma
D. ya watu wazima.

**44.** Maneno **'jambo usilolijua ni usiku wa giza'** yametumia fani gani ya lugha?
A. chuku B. tashhisi
C. istiara D. tashbihi

**45.** Watoto wanaozungumziwa katika kifungu hiki waliharibika kutokana na jambo hili hasa?
A. Kutorekebishwa na wazazi
B. Kupewa mahitaji yote
C. Wazazi kuwabwekea wachokozi
D. Kuishi maisha ya kifahari

**46.** Watoto wa Bwana Limbuka walikuwa;
A. safi, jasiri, werevu, wasiokuwa na undani
B. waigizaji, wazembe, waropokaji, walanguzi wa dawa za kulevya
C. waigaji, wasiokuwa na heshima, wazembe, walevi
D. wakakamavu, wenye bidii, waigaji, werevu

**47.** Kwa nini watoto wa Bwana Limbuka walishangaa walipoona watu wakipanda 'matatu" au "mabasi"?
A. Haikuwa kawaida matatu na mabasi kuonekana katika eneo hilo.
B. Haikuwa kawaida watu kupanda matatu na mabasi katika eneo hilo.
C. Kwa kawaida watoto hao walisafiri katika magari ya kifahari.
D. Matatu na mabasi kwa kawaida yalikuwa ya kusafirisha mizigo.

**48.** Kulingana na aya ya mwisho, **si kweli** kuwa;
A. watoto wa Bwana Limbuka hawakupita mitihani yoyote shuleni.
B. watoto wa Bwana Limbuka hawakufika katika chuo kikuu.
C. watoto wa Bwana Limbuka walijaribu kufanya biashara lakini wakashindwa.
D. watoto wa Bwana Limbuka walizunguka huku na huko bila la kufanya.

**49.** Kulingana na kifungu hiki, mtoto anafaa;
A. kujiepusha na tabia ya kuwategemea wazazi wake kwa lolote.
B. kukuzwa kwa kuzingatia makuzi yote ya kale.
C. kupewa mwelekeo wa kuzingatia maadili yanayokubalika katika jamii.
D. kufunzwa kufanya kazi nyingi mapema.

**50.** Kifungu hiki kinasisitiza umuhimu wa;
A. kuipenda na kuijali familia
B. kuzingatia malezi bora
C. kuzingatia mila na itikadi za kiafrika
D. kuwaelimisha watoto.